

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



**HALMASHAURI YA MJI IFAKARA**

**TANGAZO LA KUMPATA MKANDARASI ATAKAYEFANYA KAZI YA  
UJENZI WA SHULE YA SEKONDARI LIPANGANGALALA KATIKA  
HALMASHAURI YA MJI IFAKARA.**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia **OR-TAMISEMI** kwa mwaka wa fedha 2023-2024 imetenga fedha kupitia program ya Elimu Sekondari [SEQUIP] kwa ajili ya ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari Lipangalala katika Halmashauri ya Mji Ifakara. Ujenzi huo utafanywa kwa mfumo wa “**MKANDARASI**” kwa kadri ya mwongozo kutoka **OR-TAMISEMI** na Waziri wa Elimu.

Hivyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Ifakara, anawatangazia nafasi za kazi kwa Wakandarasi wote wenye uwezo, sifa na uzoefu wa kufanya kazi za ujenzi wa majengo kama vile; kujenga, kupaua, kupiga plasta, kufanya “wiring” kuweka vigae, kupaka rangi, kuweka milango, madirisha na umaliziaji [finishing] n.k kwa ubora wa hali ya juu wa viwango vya Serikali.

**SIFA ZA MWOMBAJI NA MASHARTI YA KAZI**

1. Awe Raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na awe na kitambulisho cha Taifa au kadi ya Mpiga kura.
2. Awe na uthibitisho wa uzoefu wa kazi za miradi ya ujenzi wa majengo kwa miradi isiyopungua [5] Serikalini.
3. Awe tayari kutekeleza kazi ya ujenzi chini ya msimamizi wa mradi [Mhandisi wa Halmashauri ya Mji Ifakara kwa kuzingatia BOQ zake.
4. Awe na uwezo wa kusoma na kutafsiri Ramani mbalimbali za majengo.
5. Awe na vifaa vya ujenzi vyenye uwezo wa kufanya kazi kama vile compactor na concrete mixer.
6. Awasilishe “Bank statement” inayoonesha kiwango cha fedha kisichopungua 100,000,000.00 katika Benki yoyote inayotambulika ikiwa na jina la Kampuni tajwa
7. Awasilishe gharama za kazi hii kulingana na maelekezo ya kazi husika kwa kujaza fomu ya gharama za mchanganuo wa kazi [BOQ]

8. Awasilishe mpango kazi na aoneshe mchanganuo wa muda halisi wa kukamilisha kila kazi atakayotakiwa kuifanya isiyozidi siku 60 za kumaliza ujenzi kwa gharama itakayokubaliwa  
9. Awe na barua ya utambulisho kutoka mamlaka ya Serikali za Mitaa, Kijiji/kitongoji au Mtaa.

10. Awe na TIN namba na Leseni ya Biashara

11. Kampuni iwe imesajiliwa kuanzia Daraja [Class] VII na kuendelea

12. Awe na Wataalamu wahandisi, mafundi sanifu na vibarua wa kutosha.

13. Awe na Mhandisi aliyesajiliwa na aliyehitimu vyuo vinavyotambulika na Serikali [Registered Engineer from ERB-Engineers Registered board katika fani yoyote ya “Civil Engineering”

14. Kampuni iwe imesajiliwa na BRELA

### **JINSI YA KUCHUKUA “TENDER DOCUMENT” NA KUTUMA MAOMBI**

Mwombaji afike Ofisi ya Halmashauri ya Mji Ifakara mkabala na Ofisi ya Tanesco Ifakara kuanzia saa **2:00 Asubuhi** hadi **saa 9:00 Alasiri** siku za kazi na ambazo sio siku za kazi ili kuchukua “Tender document” ambayo itauzwa kwa gharama ya Tsh.150,000/= baada ya kupata namba ya malipo [control number] kutoka kwa Mhasibu mkuu wa Halmashauri.

Na afike muda huo huo kwa siku zote za kazi na zisizo za kazi ili kupata ufafanuzi wa kazi, maelezo ya ziada na kuona eneo la kujenga .

Muombaji akishajaza “Tender document” aambatanishe barua ya kuomba kazi na kisha azifunge vizuri kwenye bahasha aiandike **Maombi ya ujenzi wa shule mpya ya Sekondari Lipangalala katika Halmashauri ya Mji Ifakara.**

Barua zote za maombi ya kazi ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Ifakara kupitia anuani ifuatayo

Mkurugenzi wa Mji,  
Halmashauri ya Mji Ifakara  
S.L.P 433  
**Ifakara**

Maombi ya kazi ya ujenzi yataanza kupokelewa tarehe **25/08/2023 saa 2:30 Asubuhi** hadi saa **9:30 jioni** na mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **05/09/2023 saa 8:30 Mchana.**  
Shughuli ya ufunguzi itafanyika siku ileile katika ukumbi mdogo wa Halmashauri ya Mji Ifakara

Tangazo limetolewa na

Lena M Nkaya  
**MKURUGENZI WA MJI**  
**IFAKARA**